**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA**


**SHULE YA SEKONDARI KOME**
**NAMBA ZA SIMU: MKUU WA SHULE- 0719404867**
**MAKAMU MKUU WA SHULE- 0788024005**
**S.L.P. 153**
**BUCHOSA- MWANZA**
**February, 2026**
Barua pepe: komesecondaryschool@gmail.com


Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi ..............................................................

S.L.P. ..............................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KOME HALMASHAURI YA BUCHOSA MKOA WA MWANZA KWA MWAKA WA MASOMO ………………….**

Mpendwa Mwanafunzi ....................................................................

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO mwaka wa masomo ……………… katika shule ya sekondari **KOME**. Mwaka wa Masomo utaanza tarehe **………………….** na unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **………………..**. Tafadhali ripoti mapema tayari kwa kuanza masomo.

Mwisho wa kuripoti shule itakuwa tarehe **……………..**.

**MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya sekondari KOME ipo katika kata ya NYAKASASA kisiwa cha KOME Halmashauri ya Buchosa Mkoani Mwanza. Shule inafikika kirahisi kwani kuna usafiri wa Magari ya Abiria kutoka kamanga ferry mpaka Nyakaliro kivukoni, Pia unaweza kutoka stendi ya Nyegezi hadi Sengerema, ukifika Sengerema kuna magari ya Abiria yaendayo hadi Nyakaliro kivukoni, ukishavuka kuingia kisiwa cha KOME chukua usafiri wa pikipiki (bodaboda) atakuleta mpaka shule ya sekondari KOME.

**1.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

Sare ya shule

a. Sare ya shule hii ni suruali mbili za rangi ya kijivu iwe na marinda mawili mbele na chini isipungue upana wa nchi 16 na iwe na turn up.
b. Shati mbili nyeupe za mikono mirefu na sweta la kijivu.
c. Sare za michezo truck suit ya dark blue, bukta nyeusi, t-shirt ya bluu, soksi nyeusi ndefu, na raba za michezo.
d. Viatu vya shule ni vyeusi vyenye visigino vifupi.

e. Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
f. Soksi jozi mbili nyeusi.
g. Tai mbili za kijivu (Kwa mzazi atakayependa zinapatikana shuleni kwa bei ya **Tsh.4,500/=)** na sweta la rangi ya kijivu.
h. Nguo za kushindia ni suruali rangi ya Dark-bluu na T-shirt ya maroon yenye kola (T-shirt Kwa mzazi atakayependa zinapatikana shuleni kwa bei ya **Tsh.13,000/=)**



*Muonekano wa rangi ya kitambaa cha suruali*

## 2.0 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

i. Ream mbili za karatasi za (photocopy A4) Double A- kwa mwaka.
ii. Vitabu vya masomo kulingana na tahasusi anayosoma.
  a) Daftari za kutosha, kalamu za bluu au nyeusi, penseli, rula na begi la mgongoni la madaftari.
  b) Cofa/ mkebe (mathematical instrument sets)
  c) Oxford English dictionary (kamusi ya kiingereza) na vitabu vingine vya kiingerza.
  d) Vitabu vya Geography
  e) Vitabu vya History
iii. Godoro la futi 2.5 Mwanafunzi aje nalo.
iv. Mashuka pea mbili rangi ya bluu, chandarua rangi ya bluu.
v. Vyombo vya chakula (sahani, kikombe, kijiko na bakuli)
vi. Ndoo mbili ndogo zenye mfuniko na kidumu cha lita 5 cha kutunzia maji ya kunywa.
vii. Vifaa vya usafi na kazi kila mwanafunzi aje na Jembe, Squeezer na Softbroom/Hardbroom.
viii. Faili (Spring file) kwa ajili ya kutunzia mitihani (Kwa mzazi atakayependa yanapatikana shuleni kwa **Tsh. 2,000/=)** na Tochi.
ix. Sabuni ya maji lita moja (01) kwa kila mwanafunzi.

## 2.1 MICHANGO MINGINE

1. Mchango wa uendeshaji wa shule **sh. 65,000/-**
2. Tahadhari **sh. 5,000/-**
3. Nembo **sh. 5,000/-**
4. Kitambulisho cha shule **sh. 5,000/-**

**Jumla ya michango ni sh. 80,000/-**

NB; Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya uendeshaji ya shule**; a/c number (NMB Bank) 31601200045** Jina la A/C **SHULE YA SEKONDARI KOME.**

NB; Unapofanya malipo hakikisha unaandika jina la mwanafunzi kwenye slip ya malipo utakayo leta shuleni.

**2.2 MAHITAJI MENGINE**

Mwanafunzi anatakiwa aje na Bima ya Afya au sh. 50,400/- kwa asiyekuwa nayo kwaajili ya kukata kwa mwaka.

**3.0 MAAGIZO**

i. Kila mwanafunzi lazima asome sheria, kanuni na taratibu za shule kwa makini na azifuate na kuzitii kutofanya hivyo ni makosa.
ii. Uvunjifu wa sheria yoyote ya shule hata kama ni ndogo kiasi gani hautavumilika.
iii. Mwanafunzi lazima ahudhurie vipindi vyote vinavyofundishwa darasani, afanye mazoezi na mitihani yote itakayotolewa. Ni kosa linaloweza kumfukuzisha shule kwa kuacha kuhudhuria vipindi na kufanya mazoezi/mitihani bila sababu ya msingi.

**3.1 SHERIA ZA BWENI**

i. Ni marufuku kwa Mwanafunzi yoyote kuchemsha/kupika bwenini aidha kwa kutumia motowa kuni, mkaa, mafuta ya taa au umeme.
ii. Bwenini ni mahali pa kulala si pakupiga kelele. Mazungumzo ya bwenini yawe ya maana na sauti ndogo, upigaji wa kelele au mayowe ni dalili ya ulevi, uhuni, fujo n.k hivyo havikubaliki.
iii. Usafi wa bweni ndani na nje pamoja na mazingira yanayozunguka bweni ni wajibu wa kila mkaaji wa bweni husika.
iv. Ni makosa kukarisha mgeni wa aina yoyote bwenini au katika eneo la bweni.
v. Vyoo vyote lazima vitumike vizuri na kuviacha katika hali ya usafi muda wote.
vi. Ni wajibu wa viongozi wa bweni pamoja na wanabweni wote kulinda sheria kwa kuzitekeleza kwa vitendo.
vii. Mwanafunzi haruhusiwi kuja shuleni na vyombo vifuatavyo; Redio, Heater, Kamera, Simu ya mkononi, kitu chochote kinachohusiana na simu, Hot pot, Walk man au kifaa chochote cha mziki, Sufuria, Pombe, madawa ya kulevya na manukato (perfume).
viii. Ni marufuku kwa Mwanafunzi yoyote kuingiza ama kula chakula chochote bwenini.

**NB; Mwanafunzi atakayekutwa na vitu tajwa hapo juu atachukuliwa hatua kali.**

**3.2 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa au utoro.
3. Kugoma au kuhamasisha mgomo
4. Kutoa lugha chafu kwa Wanafunzi wenzake, Walimu, Walezi na Jamii kwa ujumla.
5. Uvutaji wa Sigara
6. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote.

7. Kufuga nywele, ndevu, kunyoa pank, kunyoa kiduku, mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawepo shuleni.
8. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
9. Kuoa, uasherati au mahusiano ya jinsia moja.
10. Kumpa mimba msichana.
11. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
12. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
13. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au kuwa na kifaa chochote kinachohusiana na simu katika mazingira ya shule.
14. Kudharau bendera ya Taifa.
15. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua'
16. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.0 VIANBATANISHO NA FOMU MBALIMBALI**

i. Fomu ya kukubali kujiunga na shule ya sekondari KOME
ii. Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) isainiwe na Daktari wa wilaya.
iii. Fomu ya taarifa binafsi za Mwanafunzi.
iv. Picha nne (4) za wazazi au ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba za simu.

NB; Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao) baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi (meseji) au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wake ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yupo mahututi hivyo kumtaka mzazi atume hela.
**TAHADHARI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO;**

- **MKUU WA SHULE- 0719404867/0620751515**
- **MAKAMU MKUU WA SHULE- 0788024005**
- **MWANDAMIZI MALEZI- 0676141309**
- **MWANDAMIZI TAALUMA- 0743776437**

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo au maagizo na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KOME SEKONDARI**

**...................................**
**WITNESS A. MKUMBWA**
**( MKUU WA SHULE)**

**SHULE YA SEKONDARI KOME**
**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KOME**

1. **Sehemu ya Mwanafunzi**

Mimi ............................................................... ninakubali nafasi niliyopewa ya kuingia kidato cha tano mwaka .......... katika shule ya sekondari Kome na nitafika shuleni bila kuchelewa. Na ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi. Nitakuwa Mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za elimu ya kujitegemea. Nitaripoti shuleni kwa muda uliopangwa kila ninapofunga likizo.

Anuani yangu ya kudumu ni ..........................................................

2. **Sehemu ya Mzazi/Mlezi**

Mimi .......................................................... nina kubali mtoto wangu ................................................................. kuchukua nafasi ya kuingia shule ya sekondari Kome.
Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule, atafika shuleni kwa tarehe iliyopangwa kila wakati. Ninakuhakikishia kuwa tutashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anaripoti shuleni kwa wakati kila muhula shule inapofunguliwa.

Anuani yangu ya kudumu ni ..........................................................

Iwapo nitahamishwa au kubadili makazi lazima nitaijulisha shule kwa maandishi.

Namba yangu ya simu ni .................................................................

**FOMU HII IJAZWE NA DAKTARI KWENYE HOSPITALI ZA SERIKALI TU.**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**KOME SECONDARY SCHOOL,**
**P.O. BOX 153,**
**BUCHOSA- MWANZA.**

**The Medical Officer,**

**.....................................**

**.....................................**

Please examine ..................................................... as to his fitness for persuing advanced secondary education at this school.

1. Hemoglobin ..........................................................................................................................
2. a) Sight ..........................................................................................................................
   b) Hearing ..........................................................................................................................
3. Blood Pressure ..........................................................................................................................
4. Sickle cell test ..........................................................................................................................
5. Deformity ..........................................................................................................................
6. Urine for sugar ..........................................................................................................................
7. Epilepsy ..........................................................................................................................
8. Heart examination ..........................................................................................................................
9. Tumors breast ..........................................................................................................................
10. Leprosy ..........................................................................................................................
11. Pulmonary tuberculosis ..........................................................................................................................
12. Asthma ..........................................................................................................................
13. Stool for routine examination ..........................................................................................................................
14. Skin disease ..........................................................................................................................

Coments ; ..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

Name .............................................................. Signature .....................................................

Designation ....................................................

Station ...........................................................

Official stamp ............................................... Date ...................................................

**SHULE YA SEKONDARI KOME**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

**SEHEMU A: TAARIFA BINAFSI**

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI ........................................................................................
2. TAREHE YA KUZALIWA ..........................................................................................................
3. SHULE YA MSINGI ALIPOSOMA ..........................................................................................
4. SHULE YA SEKONDARI ALIYOSOMA ..................................................................................
5. TAHASUSI (COMBINATION) ANAYOSOMA .......................................................................

**SEHEMU B: TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

1. JINA LA MZAZI/MLEZI ........................................................................................
2. MAHALI ANAPOISHI ........................................................................................

   MTAA/KIJIJI ..........................................................................................................

   WILAYA ..................................................................................................................

   MKOA ......................................................................................................................
3. NAMBA YA SIMU ................................................. AU ............................................